

Jedwali la Kazi ya Uchambuzi wa Vigawanyi na Viunganishi vya RAPID 1

Tathmini hii ya **Uchambuzi wa Vigawanyi na Viunganishi vya RAPID** ni muhimu sana kufanya na kikundi tofauti. Jedwali la pili ya kazi inaweza kutumika kujibu maswali yaliyo hapa chini.

HATUA YA 1: JADILI

Tengeneza Orodha ya Vigawanyi na Viunganishi Kwa Kutumia Jedwali la Kazi ya Uchambuzi wa Vigawanyi na Viunganishi. Maswali hapa chini yanaweza kutumika kama mwongozo wa kufanya tathmini ya awali katika muktadha wako.

- | | |
|---|--|
| <ul style="list-style-type: none"> • Mmambo gani ni vigawanyi katika hali hii? (Mambo gani yanapinga amani au kuchangia migogoro?) • Je, hii vinagawanya watu kiviipi? • Kwa nini ni muhimu? • Ni mambo gani, masuala au vipengele gani vinasababisha migogoro na kugawanya watu? Na ni jinsi gani? • Je, ni vitisho gani vya sasa vinaharibu amani na utulivu? • Ni mambo gani hatari zaidi katika hali hii? (Kigawanyi hiki ni hatari kiasi gani?) • Ni nini kinachoweza kusababisha mvutano kuongezeka katika hali hii? • Nani anaongoza katika kuharibu amani/kwa kuchangia migogoro na kwa njia gani? • Ni watu gani au makundi gani katika hali hiyo yana uwezo wa kuathiri sana mgogoro huo kwa njia mbaya? • Je, kuna vigawanyi vinavyohusishwa na majukumu ya kijinsia au vikundi vilivyopangwa vya wanaume, wanawake, au vijana? Je, vikundi fulani vinateseka zaidi kuliko vingine katika hali hiyo—na hii ina athari gani kwa viwagawanyi? Ni mambo gani yanaunganisha katika hali hii? (Je, ni mambo gani ya sasa katika hali hiyo ambazo zinaweza kutumiwa kuinua hali ya amani?) | <ul style="list-style-type: none"> • Je, haya yanaunganisha watu vipi? • Kwa nini ni muhimu? • Ni nini kinacholeta watu pamoja katika hali hii/katika mistari ya migogoro? (Kiunganishi hiki kina nguvu kiasi gani?) • Je, ni usaidizi gani wa sasa ni wa amani na utulivu? • Watu hukutana wapi? Je, watu hufanya nini pamoja?? • Watu hushirikianaje? • Ni watu gani au vikundi gani katika hali hiyo viko katika nafasi ya kushawishi mzozo kwa njia ipasavyo? • Je, kiunganishi hiki kina uwezo? • Je, kuna viunganishi vinavyohusishwa na majukumu ya kijinsia au vikundi vilivyopangwa vya wanaume, wanawake au vijana? Je, vikundi fulani vinateseka zaidi kuliko vingine katika hali hiyo—na ni nini madhara ya hili kwa viunganishi? |
|---|--|

HATUA YA 2: JADILI

Hii ni hatua muhimu ya kuhalalisha Vigawanyi na Viunganishi vyako kabla ya kuanza kuipa kipaumbele ni zipi unataka kuzingatia katika mradi wako.

Je, hivi ni **vigawanyi vinavyofaa**?

- Tunajuaje kuwa havi ni viwagawanyi?
- Je, hizi ni sababu zilizopo?
- Tungejuaje ikiwa haya yalibadilika? (viashirio)

Je, hivi ndivyo **viunganishi sahihi**?

- Tunajuaje kuwa hizi ni viunganishi?
- Je, hizi ni sababu zilizopo?
- Tungejuaje ikiwa haya yalibadilika? (viashirio)

HATUA YA 3: WEKA KIPAUMBELE

Hakuna vigezo vya jumla vya kuipa kipaumbele. Badala yake, unaifanya kwa kile ambacho wadau wanaamini kuwa ni kweli mashinani na kwa mitazamo yao (yaani, kulingana na vigezo vyao). Kwa maneno mengine, ni nini kinachozuia uhusiano mzuri na uaminifu zaidi kutoka kwa mtazamo wao?

- Vigawanyi gani ni muhimu au hatari zaidi?

- Ni viunganishi gani muhimu zaidi, imara au vyema zaidi?

Jedwali la kazi 2 b: Jedwali la Kazi ya Uchambuzi wa Vigawanyu na Viunganishi 2

Chati hii inaambatana na ile jedwali la kazi iliyotangulia na inaweza kutumika kujibu maswali yaliyo hapo juu.

	VIWAGAWANYI	VIUNGANISHI
HATUA YA 1: JADILI		
HATUA YA 2: JADILI		
HATUA YA 3: WEKA KIPAUMBELE		